# JINSI YA KUANZISHA MAKTABA NDOGO YA JUMUIYA

**Kuelekea Kuleta Mwamko Mpya wa Kujisomea Tanzania**

***Na. B. Godfrey a.k.a M. M. Mwanakijiji***

**Novemba 20, 2014**

**Utangulizi**

Mataifa yote ambayo yameweza kupiga hatua za haraka za maendeleo ni mataifa ambayo yameweka mkazo mno katika elimu; katika kusoma; katika kupata maarifa. Tangu enzi za Wagiriki wa kale hadi leo hii jamii ambazo zimeweza kujibadilishia kwa haraka na kwa ubora maisha yao ni jamii ambazo kati yake kulikuwepo na kuthamini vitabu. Hii ni kweli kuanzia Uchina, Ulaya, Marekani, India na hata Afrika. Hata mabadiliko makubwa yaliyosababishwa na ujio wa Mapinduzi ya Viwanda yanaweza kuhusishwa moja kwa moja na upatikanaji wa vitabu kwa urahisi zaidi na kwa watu wengi zaidi.

Upatikanaji wa vitabu katika jamii mbalimbali ulisababisha uharaka na urahisi wa kupatikana maarifa kutoka jamii moja kwenda jamii nyingine. Hata wakati baadhi ya tawala za nchi za Kikristu za Ulaya zilipokuwa katika kinachoitwa na baadhi ya wanahistoria kuwa ni Zama za Giza (Dark Ages) baada ya kuporomoka kwa utawala wa Kirumi na kupungua sana kwa upatikanaji wa maarifa nchi nyingine za Bara la Arabia zilikumbatia vitabu na elimu. Hii ni kweli kwani wakati Ulaya kunaporomoka katika maarifa nchi za Uarabuni za Kiislamu Mashariki ya Kati zilikuwa zinazama katika kukumbatia maarifa ambayo waliyapata kutoka katika vitabu vya Wagiriki wa kale. Hii iliendelea tena hadi ilipogeuka kwa mwamko tena wa Ulaya na kudidimia kwa nchi za Kiarabu nakuinka tena kwa nchi za Magharibi kuelekea kwenye karne ya 15.

Njia kubwa ya kuhakikisha kuwa maarifa ya kila namna yanapatikana kwa urahisi na yanawafikia watu wengi ilikuwa ni kutengeneza mahali ambapo watu – wasomi na wasio wasomi – wangeweza kufikia vitabu na kusoma. Ndio maana hadi leo baadhi ya maktaba za kale kabisa bado zinafanya kazi huku nyingine zinakumbukwa tu kwa mchango wake. Maktaba za kale zinazojulikana ni pamoja na ile ya Alexandria (Misri) na ile ya Constantinople (Uturuki). Lakini pia zipo nyingine ambazo hazijapata umaarufu kama hizi na zinadumu ikiwemo ile ya Timbuktu (Mali) au zile za Chingueti (Mauritania).

Siyo lengo langu kuandika kwa kirefu juu ya historia ya maktaba katika Tanzania. Itoshe kusema tu kuwa tangu wakati wa ukoloni suala la kuanzisha maktaba ili kufikisha maarifa na elimu kwa watu wengi zaidi lilitiliwa mkazo kwa kiasi chake. Tatizo kubwa sana ambalo Tanzania (Tanganyika wakati huo) ilikutana nalo katika kufadhili miradi ya maktaba ni kuwa Tanganyika halikuwa koloni kama Kenya au Uganda bali ilikuwa ni Eneo la Uangalizi (Mandate Territory) ambapo Uingereza ilipewa baada ya Ujerumani kushindwa vita ya kwanza ya dunia.

Mojawapo ya Maktaba nzuri kabisa kuanzishwa kabla ya Uhuru ni ile ya Tanga iliyoanzishwa kama Maktaba ya Kumbukumbu ya Mfalme George VI. Maktaba hii ilianzishwa mwaka 1958 na utawala wa Mwingereza. Maktaba hii ilikuwa ni miongoni mwa maktaba nzuri kabisa; ilianza ikiwa na vitabu kama 7000 hivi hadi ilipokuja kugeuzwa kuwa Maktaba ya Tanga (mwaka 1964) ikiwa na vitabu zaidiy ya 15,000. Hata ilipoundwa Bodi ya kwanza ya Maktaba chini ya Sheria ya Maktaba ya 1963 na baadaye Sheria ya Maktaba ya 1975 Maktaba ziliendelea kujengwa sehemu mbalimbali nchini – za binafsi na za serikali, kwenye vyuo na hata kwenye shule mbalimbali.

Hata hivyo usomaji na matumizi ya maktaba nchini bado ni wa chini sana kulinganisha na mataifa yaliyoendelea au ambayo yako kwenye mpaka wa kuendelea. Zipo tafiti ambazo zinaonesha jinsi gani matumizi ya maktaba hayako juu sana isipokuwa kwa baadhi ya miji na maeneo ambapo wanafunzi wanatafuta mahali pa kujisomea au kupotezea muda. Kutokana na sababu hizi na nyingine nyingi matumizi ya maktaba hayako miongoni mwa vipaumbele vya watu; ukiondoa wale ambao wako vyuoni ambako wanatarajiwa kuwa watatumia maktaba. Nje ya shule na vyuo maktaba bado ni kama anasa (luxury) fulani.

Kijitabu hiki kina lengo la kukabiliana na tatizo hili; la idadi ndogo ya maktaba zilizopo na pili tabia ya kutopenda kujisomea ambayo inaonekana imekuwa kama sehemu yetu ya jamii.

**TATIZO LA MSINGI**

Tatizo la msingi ambalo lipo kutokana na matumizi ya maktaba ni umbali wa maktaba hizo na zaidi pia uwepo wa vitabu vya kisasa na vinavyoenda na wakati. Wakati baadhi ya maktaba zimefadhiliwa vya kutosha lakini bado maktaba hizo hazijawafikia watu wengi na kiukweli haziwezi kuwafikia watu wengi. Kwa mfano jiji la Dar lina Maktaba moja kubwa ya Umma (Maktaba Kuu) huku maktaba nyingine nyingi zikiwa ni zile za vyuo na shule mbalimbali au zile zinazoendeshwa na Ofisi za Kibalozi. Wananchi wengi hata hivyo hawana ile nafasi au hata hawaoni umuhimu wa kwenda maktaba kwani kwa wengine maktaba ni kama mahali pa wasomi fulani – mahali pa kwenda kufanya utafiti.

Pia lipo tatizo la gharama kubwa ya kutengeneza na kuendesha maktaba ya kisasa. Zamani maktaba ilikuwa ni kuhusiana na vitabu tu; leo hii maktaba ni zaidi ya vitabu. Maktaba ni mitandao na njia nyingine za kisasa za kupashana habari. NI kwa sababu hiyo maktaba za zamani zilizojengwa baada ya 1964 katika mikoa na wilaya mbalimbali nyingi hazijafanyiwa matengenezo makubwa ya kuzileta katika ulimwengu wa karne ya ishirini na moja. Majengo yake yamechangaa na kama ni matengenezo ni yale ya kuziba viraka. Licha ya ongezeko la watu maktaba hizi nyingi hazijafanyiwa upanuzi wenye kuendana na mahitaji ya watu kwani bado watu wengi hawazitumii na hivyo hazionekani kama zinahitaji matengenezo haya. Licha ya kuongeza shule nyingi sana na wanafunzi wengi bado huduma ya maktaba iko chini kulinganisha na mahitaji ya watu.

Hili ni tatizo ambalo sioni namna gani serikali ambayo vipaumbele vyake vinakinzana sana inaweza kulishughulikia kwa haraka. Ni jukumu la wananchi wenyewe kujionesha kuwa wanapenda na kuthamini vitabu.

Katika uchunguzi wangu wa haraka haraka sioni kama katika tawala zote zilizofuatia baada ya Baba wa Taifa kuna ambayo imejenga maktaba mpya za umma tena za kisasa ukiondoa zile za kwenye vyuo na mashule. Maktaba karibu zote zilizopo sasa – zile za Mkoa na zile ambazo ziko kwenye baadhi ya Wilaya zimejengwa wakati wa utawala wa Mwalimu au zilirithiwa toka kwa wakoloni. Ndiyo maana wakati mwingine tunaposikia watu wanajisifia kuthamini elimu wengine

tunabakia kujiuliza kama wanapima vipi uthamini wao wa elimu hasa kama hawajawahi kukanyaga mguu hata maktaba moja au kujenga angalau maktaba moja ya mfano.

**HAJA YA KUWA NA MAKTABA ZA JUMUIYA**

Mwongozo huu una lengo moja kubwa; kuwasaidia wale wote wenye kupenda vitabu na wanaopenda kurithisha maarifa yanayopatikana kwenye vitabu kujaribu kuanzisha na kuendesha maktaba ndogondogo za jumuiya ili kuwezesha kuwafikia watu wengi zaidi ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza wasifikiwe na vitabu.

Hivyo, maktaba ya jumuiya basi ni *maktaba ambayo imeanzishwa na jumuiya ili kukidhi mahitaji ya kupatikana vitabu vya aina mbalimbali kwa ajili ya kuazima ili kujisomea au kufanya rejea (reference).* Maktaba ya jumuiya huweza kuanzishwa na taasisi, mtu mmoja au kikundi cha watu wote wakiwa na lengo la kuchochea usomaji wa vitabu kwa makundi mbalimbali ya watu. Tofauti kubwa ya maktaba ya jumuiya (community library) na maktaba ya umma (public library) ni kuwa maktaba ya umma huanzishwa na kuendeshwa kwa gharama za walipa kodi na huendeshwa na kitendo au idara ya umma wakati maktaba za jumuiya huanzishwa na kuendeshwa nje ya mamlaka ya kiserikali hata kama inafuata muongozo fulani wa kiserikali. Maktaba ya jumuiya basi inaangukia upande wa maktaba za binafsi.

Maktaba ya Jumuiya kimsingi siyo kubwa sana na hazihitaji gharama kubwa ya uanzishwaji au uendeshaji; bali zinahitaji vitu viwili vikubwa muda na moyo wa kujitolea (time and commitment). Mtu au kikundi cha watu wanaotaka kuanzisha maktaba ya jumuiya ni lazima wawe tayari kujiandaa mapema, kujipanga na kuwa tayari kujikuta wameshika tama kwenye kona ya kukata tamaa na kushindwa. Kuanzisha maktaba ya aina hii inahitaji moyo wa kutokukata tamaa.

Maktaba za jumuiya zinaweza kuanzishwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya usomaji wa vitabu kwa ujumla (general book reading) au kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya vitabu maalum; kwa mfano maktaba za kidini au za fani fulani ya elimu. Hata hivyo kwa ajili ya mwongozo huu unafikiria zaidi maktaba ya jumla ambayo itakuwa inaweza kuhudumia kuanzia watoto na hata watu wazima. Hatufikirii sana maktaba ya kisomi (academic library) bali zaidi maktaba ya kujisomea vitabu mbalimbali.

**Lengo la Maktaba za Jumuiya ni nini?**

Kama zilivyo maktaba nyingine zote kuna malengo makubwa yafuatayo ya kuanzisha maktaba ya jumuiya:

- Maktaba inasaidia wanafunzi kufanya vizuri shuleni kwa kuwapatia mazingira mazuri ya kujisomea na pia kuwapatia vitabu zaidi vya kujifunzia;
- Maktaba inatoa nafasi kwa wanaojifunza kusoma kufanya mazoezi ya kujisomea vitabu vya aina mbalimbali na vya ngazi mbalimbali;
- Maktaba inaleta maarifa mapya katika jamii kwa kufikisha vitabu vya maarifa mbalimbali ambayo siyo rahisi kupatikana katika shule au chuo au katika darasa

rasmi. Mtu kwa kujisomea anaweza kupata maarifa ambayo asingeweza kuyapta bila hilo;

- Maktaba inatumika kama hifadhi ya ujuzi na maarifa katika jamii. Siyo lazima vitabu vilivyopo viwe kutoka nje; hata kazi za waandishi wa ndani au katika jamii ile ile zinaweza kupatikana katika maktaba hiyo. Karibu maktaba nyingi za nchi kama Marekani zina nafasi kwa waandishi na watunzi wa eneo lao kuonesha kazi zao;
- Maktaba ni mahapo pa burudani vile vile; baadhi ya maktaba za jamii hutoa nafasi kwa kufanyika burudani mbalimbali kwa wanafunzi hata watu wengine. Hata maktaba ndogo za jumuiya zinaweza kupanga maonesho ya kazi mbalimbali za fasihi na Sanaa;
- Maktaba zinatumika pia kuwa sehemu ya kutolea mafunzo mbalimbali ikiwemo elimu ya watu wazima au mafunzo kwa watoto. Masimulizi ya hadithi na vitendawili yanaweza kufanyika katika mazingira ya maktaba;
- Hizi ni sehemu tu ya faida za kuwa na maktaba – ndogo au kubwa katika jumuiya. Faida nyingine kubwa zinaweza kupatikana katika maktaba kubwa zaidi.

## HATUA ZA KUANZISHA MAKTABA

Kabla mtu au kikundi cha watu hakijaamua kama kinaweza kuanzisha maktaba yake ni vizuri kijiuliize maswali kadhaa ili kuweza kuona kama wazo zima linawezekana au haliwezekani. Baadhi ya Maswali ya kujiuliza ni haya yafuatayo:

- Je, kusoma vitabu ni muhimu kwangu?
- Je, ningependa kuona watu wengi zaidi bila kujali rika lao wanapenda kusoma vitabu mbalimbali?
- Je, jamii yangu ina mwamko wa kusoma vitabu na kama upo ni kwa kiasi gani na kama haupo yawezekana kwanini?
- Je, naweza kutumia muda, raslimali na vipaji vyangu kuanzisha maktaba ndogo ya kujisomea?
- Je, kuna watu wengine katika jumuiya ambao naweza kuwashirikisha wazo hili na wanaweza kuunga mkono kwa namna mbalimbali?
- Je, jumuiya yangu ina watoto wengi wa umri wa kwenda shule au watoto wadogo; vipi kuhusu wanafunzi wa vyuo na wafanyakazi?
- Je, naweza kuhusisha watu wengine katika jumuiya ambao tunaweza kushirikiana kuanzisha maktaba?

Swali hili la mwisho ni la muhimu sana katika kuamua kama maktaba inaweza kuanzishwa. Ni muhimu hapa tuangalie basi njia mbili zinazotegemea jibu la swali hilo la mwisho. Kama wazo la maktaba linaungwa mkono na watu wengi na wapo wengine ambao wako tayari kushirikiana basi maktaba itakuwa ni ya jumuiya kweli. Hata hivyo kwenye mazingira ambapo ni vigumu kuhusisha watu wengi maktaba itakuwa zaidi ni ya kifamilia ambapo wahusika wake ni ndugu na jamaa wa karibu. Njia zote mbili zaweza kufaa; kuwa na maktaba ndogo ya jumuiya au kuwa na utaratibu wa

kuazimana vitabu nje ya maktaba. Katika safu hii hata hivyo nitajikita katika kuanzisha maktaba ya jumuiya. Labda baadaye nitaweza kuandika juu ya kuanzisha utaratibu wa kuazimana vitabu bila ya kuwa na maktaba.

### KUANZISHA MAKTABA KWENYE JUMUIYA

Maktaba ndogo ya jumuiya inaweza kuanzishwa mahali popote ambapo mtu, taasisi au kikundi cha watu kimeamua na pana mazingira mazuri ya kuweza kuhifadhi vitabu katika hali ya ubora na usalama. Maktaba ya aina hii inaweza kuanzishwa kwenye mtaa au kitongoji, kijiji, kata n.k. Kwa vile maktaba hii ina lengo la kuwa sehemu ya jumuiya basi inaweza kuwa katika ngazi ya mtaa na kitongoji au hata kijiji. Na kwa vile ni maktaba itakayoendeshwa kwa kujitolea zaidi basi si vizuri kufanya ihudumie jamii kubwa. Wakati wowote pale ambapo ipo haja ya kupanua uwezo wake basi maktaba nyingine ndogo inaweza kuanzishwa kuhudumia jumuiya nyingine. Kama inabidi sana kuna uwezekano wa kuanzisha hata ushirikiano wa maktaba hizi ndogo ndogo za jumuiya hasa pale ambapo tayari zimejijenga katika jamii.

### Kamati /Bodi ya Maktaba

Kitu cha kwanza kabisa kuelekea kuanzisha maktaba ya jumuiya ni kuunda timu ya watu wachache ambao watakuwa ndio nanga ya uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba hiyo. Timu hii itafanya kazi kama Kamati au Bodi katika kuhakikisha kuwa mpango mzima unafanikiwa. Kamati hii inaweza kuwa na idadi yoyote ya watu kulingana na mahitaji. Hata hivyo, ili kuleta ufanisi ni vizuri ikahusisha watu wachache ambao kweli wana kiu ya kuleta maarifa katika jamii na wanao muda wa kufuatilia hili. Haifai kuwashirikisha watu ambao hawataweza kutoa muda wao kutimiza lengo hili la kuwa na maktaba.

Kamati hii inaweza kuwa na:

***Mwenyekiti*** – Kiongozi na mtendaji mkuu wa mradi huu na ambaye atakuwa anawajibika kuongoza vikao vya kamati.

***Makamu Mwenyekiti*** – Msaidizi wa karibu wa Mwenyekiti na atakaimu nafasi ya Mwenyekiti wakati hayupo. Anaweza kupewa majukumu mengine mbalimbali na Mwenyekiti au kikao.

***Katibu*** – Afisa wa Kamati ambaye atakuwa na wajibu wa kuandika taarifa mbalimbali za vikao, kuandaa ajenda na majukumu mengine ya kamati. Ni vizuri awe ni mtu mwenye uwezo mzuri katika mambo ya uandishi.

***Mweka Hazina*** – Atakuwa na wajibu wa kutunza fedha za Maktaba na kuhakikisha zinatumika inavyopaswa; kuandaa taarifa za fedha n.k Ni vizuri awe mtu mwenye ujuzi wa msingi katika masuala ya utunzaji wa kumbukumbu za fedha (accounting).

***Mktubi*** – Huyu atakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za maktaba; ndiye mtu ambaye atakuwa sura ya maktaba kwa wanajumuiya.

Jinsi gani viongozi hawa wanapatikana inaweza kutofautiana mahali na mahali. Hata hivyo, kwa vikao vya mwanzo wale waanzilishi na yule muasisi atakuwa ndiyo mwenyekiti wa muda na wenzake watakapokutana katika kikao cha kwanza watamthibitisha au watamchagua mtu mwingine kuwa mwenyekiti wa kikao au vikao vya kwanza vya kujipanga.

Jukumu la vikao vya kwanza ni kujadiliana suala la kuanzisha maktaba ya jumuiya na kuona kama kila mmoja yuko katika uelewa ule ule. Pamoja na mipango hiyo vikao hivyo vya kwanza vitaandaa mwongozo wa kamati au kanuni za maktaba. Hii ni vizuri kuweka utaratibu huu mapema kabla ya kuanza ili kila mtu ajue vizuri na kwa wazi kabisa utaratibu ukoje, uongozi unafanyaje kazi, uongozi unabadilishwaje n.k Taratibu hizi zinaweza kuwa katika mfumo wa *Articles of Association*.

**HATUA ZA KUANZISHA MAKTABA**

Baada ya kuwa na mwongozo basi maamuzi ya uanzishwaji wa maktaba yanaweza kufanyika. Ili kufikia kuanzisha maktaba inayoweza kufanya kazi basi hatua zifuatazo ni muhimu kufuatwa na wahusika kujiridhisha.

**1. Mahali**

Hakuna uamuzi mkubwa na wa msingi kabisa ambao unaweza kuamua kama maktaba itafanikiwa au la kama mahali ambapo maktaba hiyo itakuwa. Kwa kuanzia maktaba inaweza kuwekwa mahali popote; na kwa vile si lazima iwe na maelfu ya vitabu, maktaba yenyewe inaweza kuanza na vitabu vichache tu kwenye kabati la kuweka vitabu (shelf). Kama maktaba inaanzishwa shuleni basi ni kuangalia inakuwa mahali gani; inaweza kuwa kwenye moja ya darasa, ofisi au kumbi ambazo ni rahisi kufikika.

La maana ni vizuri kuhakikisha mahali popote ambapo vitabu vitatunzwa patakuwa salama, pasafi na pana nafasi nzuri ya watu kuweza kuingia na kutoka. Maktaba ikiwa imejificha sana itakuwa vigumu kwa watu kufikia; hivyo ni muhimu eneo (location) ifikiriwe kwa kina. Hata kama ni nyumbani kwa mtu ni vizuri kuhakikisha kuwa haitoingilia shughuli au maisha ya mtu nyumbani kwake.

Kwenye maeneo ambayo labda chumba au ukumbi ni vigumu kupatikana watu wanaweza kufikiria kuwa na makabati ambayo yanaweza kutolewa nje na kupangwa vitabu mara moja kwa wiki na watu wakaja na kuazima vitabu. au kurudisha vitabu na makabati hayo kurudishwa kuhifadhiwa ndani hadi wiki nyingine.

Ili kuamua hili ni vizuri kuhakikisha waandaji wanazungumza na watu mbalimbali kuona kama wanaweza kutoa nafasi ya kuweka maktaba. Mfano, kwenye Parokia, Msikiti, Hospitali, Shule, Ofisi n.k. Katika maeneo yetu kuna sehemu nyingi ambazo zina nafasi na zinazoweza kutumika kama kama maktaba. Binafsi nakumbuka tulipoanzisha maktaba ndogo kwenye Parokia ya Mt. Francis Xavier Nyakahoja Mwanza, miaka ya tisini tulitumia ukumbi ambao zamani ulikuwa ni stoo ya vitu mbalimbali. Baada ya kutembelea sehemu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kama maktaba basi kamati itaamua sehemu bora zaidi.

**Fikiria kutumia Makontena Yaliyotumika Kama Maktaba**

Mojawapo ya maeneo mazuri sana kuanzishia maktaba ya jumuiya ni kununua kontena lililotumika na kulibadilisha kutengeneza maktaba. Mkiweza kununua mawili tu yanatosha kabisa kuwa na maktaba ndogo, na ofisi ndogo na hata kutengeneza sehemu ya kujisomea au kufanya shughuli mbalimbali. Kwa jiji la Dar kwa mfano kontena linaweza kununuliwa kwa chuini ya dola 1000; ni kiasi kidogo sana kulinganisha na kuamua kujenga jengo zima!

Picha hizi ni Mifano ya Makontenda Yanavyoweza kuwa Maktaba









Hata kwa gharama ndogo unaweza kufanya maktaba ikawa 'special' kweli kweli



Au ya kawaida kabisa



Kama sehemu iliyochaguliwa inahitaji kufanyiwa matengenezo kidogo au hata kupaka rangi basi wadau wa ile maktaba watapaswa kujipanga na kujitolea kufanya kazi hiyo. Ni vizuri kama kazi ya kusafisha, kupanga na kupamba maktaba hiyo ndogo ikafanywa na wanachama wenyewe; hii itawafanya waione ni ya kwao, waitunze na kuilinda. Itakuwa siyo tu ni zao la akili zao bali pia ni matokeo ya jasho lao.

### 2. Kupata Vitabu na Vitu vya Kuazimana

Vitabu ndivyo vitakuwa vitu vitakavyojaza zaidi maktaba ili watu waazime. Hata hivyo, watu wanaweza kuazima filamu na muziki katika CD, DVD, Mabango, Vifaa vya kufundishia, Ramani, na sehemu nyingine hata zana za kazi. Kwa vile maktaba ya aina hii ni ya kujitolea ni wazi kuwa sehemu kubwa ya raslimali yake itatoka kwa wadau wenyewe. Hivyo, ni muhimu kujiuliza kwanza kabisa ni vitabu vya aina gani vinahitajika pale. Kwa mfano, kama eneo lina watoto wengi wa chini ya umri wa kwenda shule, au wa shule ya msingi basi ni wazi vitabu vya kuchochea usomaji wa awali vitakuwa ni vya muhimu na msaada mno kwa wazazi. Mahali ambapo pana wanafunzi wengi wa Sekondari basi vitabu vingi vya sekondari vitakuwa vinahitajika. Mahali ambapo pana wafanyakazi wengi n.k basi mahitaji ya vitabu yataendana na mahitaji ya vitabu vya watu wazima. Na mahali penye mchanganyiko mkubwa ni wazi utahitaji kuwa na vitabu vya aina nyingi.

Chanzo cha kwanza kabisa cha vitabu hivi ni wanajumuiya wenyewe. Wengi wetu tuna vitabu vingi ambavyo vimerundikana ndani au hata kwenye maktaba zetu wenyewe (japo hata kama hatusomi vimekaa kama mapambo). NI vizuri kuangalia ni kwa namna gani kila mmoja ataanza kwa kuchangia vile alivyonavyo. Ni lazima kuwa na kanuni ya vitabu gani mnaweza kukusanya (collection policy). NI vizuri viwe vitabu ambavyo havijachafuliwa; visiwe na alama alama nyingi ndani, na viwe na maganda yake ya juu.

Kutoka kwa wadau kamati inaweza ikaomba misaada ya vitabu kwa wadau wengine wa usomaji, makampuni na taasisi na pale inapowezekana watu wakanunua baadhi ya vitabu vipya hasa kwa mahitaji ya wanafunzi. Kuna taasisi nyingi za kimataifa hasa katika nchi zilizoendelea ambazo hutoa misaada ya vitabu katika Afrika. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa mahali popote mnapoomba misaada ya vitabu wajue mapema juu ya sera yenu ya vitabu mnavyokusanya. Si vizuri kukubali kila kitabu ilimradi kimetolewa msaada! Lakini pia kwa vile maktaba ni sehemu ya ujuzi si vizuri kuweka vitabu vya mtazamo wa aina moja tu.

Kwa wale ambao kati yao kuna taasisi za kidini kwa mfano, utaratibu unaweza kuweka na viongozi hao wa kidini kuweka maboksi ambapo watu wenye vitabu vya ziada ambavyo vinazingatia masharti ya ukusanyaji kuvichangia. Unaweza kushangaa jinsi watu wanavyoweza kujitolea kutoa vitabu na ni vitabu vya aina gani vinaweza kupatikana. Kwa mfano, watu wengi wanaosafiri hupenda kununua vitabu wanavyosoma safarini na wanaporudi nyumbani wanakuwa wamevimaliza na kuviweka ndani tu.

Mojawapo ya mambo mazuri sana ya kutosahau kufanya kwa maktaba yoyote ya jumuiya ni kuwashukuru wadau na wafadhili wake – wawe wale wa ndani na wale wan je. Shukrani zinaweza kuwa katika barua au hata kwa kuweka majina ya wadau hao katika mfumo wa kumbukumbu kama vibao vyenye kushukuru mchango wao.

Mojawapo ya njia nzuri za kuanzisha maktaba kama hizi ni kuwasiliana na waktubi (librarians) ambao wanaweza kutoa mchango wa mawazo n ahata misaada ya vitabu kwa kuviazimisha kwenye maktaba yenu kwa muda. Hivyo, ni vizuri hata kutembelea maktaba zilizopo tayari kuona jinsi gani zinaweza kusaidia. Njia nyingine pia kuwasiliana na balozi mbalimbali au makampuni ya kimataifa yanayofanya kazi nchini; wengi wa hawa wana vitabu vingi katika hazina zao na wanaweza kabisa – tena kwa furaha – kutoa baadhi ya vitabu kama misaada.

Nyingine ni kuwasiliana na vyuo vikuu ambavyo mara nyingi hupokea misaada ya vitabu mbalimbali. Wakati mwingine baadhi ya vitabu wanavyopokea si kwa matumizi ya vyuo vikuu zaidi (kwa mfano vitabu vya watoto na vya elimu ya msingi). KUwasiliana nao na kuulizia kunaweza kufungua mlango mwingine wa vitabu. Hili ni kweli hata kwenye taasisi za kidini, wizara na idara mbalimbali.

Siyo tu vitabu hata kompyuta za zamani kidogo zinaweza kutolewa kama msaada na maktaba yenu ikawa na sehemu ambapo watu wanaweza kuja na kutumia kompyuta au intaneti bure kama wanachama.

### 3. Masuala ya Fedha

Japo sehemu kubwa ya uendeshaji wa maktaba hii itakuwa ni kwa kujitolea hata hivyo ni wazi kuwa kuna wakati gharama ya fedha itahitajika. Zipo gharama nyingine ndogo ndogo zinazoweza kuhitajika na hili maktaba itahitaji kuliwekea utaratibu. Gharama kwa mfano za usafirishaji, kutengeneza makabati, kulipia bili mbalimbali n.k. NI kwa sababu hiyo ni vizuri kuwa na utaratibu wa masuala ya fedha, bajeti na kusimamia matumizi vizuri.

Hivyo, ipo haja ya kuangalia jinsi ya kuanzisha akaunti na kuendesha akaunti ya maktaba. Kwa vile mradi mzima kwa kiasi kikubwa ni wa kujitolea na ni vizuri kufikiria kujitegemea vile vile taratibu za kuchangisha fedha zinaweza kutumika. Mojawapo ya vitu ambavyo ningependa sana kuvikatisha tamaa ni kutegemea fedha kutoka nje ya nchi au kwa misaada ya 'wafadhili'. Ni vizuri wafadhili wawe ni wanajumuiya wenyewe kwa kiasi chote wanachoweza; hili litafanya waone ile umiliki wa maktaba yao.

Ni vizuri kuzingatia na kufuata kwa makini kabisa kanuni na utaratibu wa manunuzi uliokubaliwa na kamati pamoja na kuzingatia kanuni za utunzaji wa vitabu vya fedha (bookkeeping). Kuandaa bajeti, kusimamia mapato na matumizi na kutoa taarifa za fedha

kwa jumuiya ni muhimu sana ili kuonesha uadilifu. Maktaba isije ikawa mradi mwingine wa watu wachache kujitafutia ulaji kwenye jumuiya badala ya kuchochea usomaji!

### 4. **Kuwa na Mktubi (Librarian**)

Maktaba ni muhimu iwe na mtu ambaye anaweza kusimamia shughuli za maktaba na ambaye ana ujuzi kidogo wa mambo ya maktaba. Huyu anapaswa kuwa mtu ambaye angalau anaweza kuwa amejifunza kidogo namna ya kusimamia na kuhakikisha maktaba inafanya kazi. Hili si jambo gumu kwani kwa muda mfupi mtu anaweza kupata ujuzi wa msingi unaohitajika kuendesha maktaba. Kwenye maktaba ndogo kama hizi za jumuiya basi Mktubi anaweza kuwa pia sehemu ya Kamati ya Maktaba. Na kwa vile ni kazi ya kujitolea ni vizuri kuhakikisha kuwa anapewa msaada wote unaohitajika.

Mojawapo ya mambo yanayowezekana ni kuwasiliana na maktaba za Serikali au Chuo kutoa mafunzo machache kwa mktubi wenu. Nina uhakika wapo waktubia ambao watafurahia na kupata moyo kuona juhudi hizo za wananchi kujisomea na watakuwa tayari kutoa msaada. Wengine wanaweza hata kujitolea muda wao kusaidia uanzishwa wa maktaba yenu.

### 5. **Kanuni za Maktaba**

Wakati upo mwongozo wa kamati ni vizuri na ni lazima kuandaa kanuni za kuendesha maktaba ya jumuiya. Hizi tunaweza kuziita ni Sera za Maktaba (Library Policies). Nani anaweza kuwa mwanachama (awe mkazi wa eneo husika kwa mfano), wa umri gani, n.k Sera zitaamua ni vitabu vingapi mtu anaweza kuazima na anaweza kukaa navyo kwa muda gani. Sera hizi zitaamua pia aina ya adhabu kwa watu ambao watachelewa kurudisha vitabu au watarudisha vitabu vikiwa vimeharibika au hawatorudisha kabisa vitabu. Kama adhabu itahusisha malipo kidogo ya fedha basi kanuni zitasema wazi kabisa ni kiasi gani kitalipwa kwa uharibifu, ucheleweshaji au upoteaji wa vitabu. Hivi juzi mwanangu mkubwa alipoteza kitabu toka maktaba ya shule; ikabidi tulipe dola nne ($4) kulipia kitabu hicho. Hiyo ikiwa gharama ya kitabu chenyewe kama ningekinunua dukani.

Na kanuni kubwa na ya msingi kabisa ni kuamua maktaba itafanya kazi siku gani na muda gani. Kwa vile maktaba hii ni ya jumuiya na inaendeshwa kwa kujitolea ni wazi haiwezi kufanya kazi siku saba, asubuhi hadi jioni. Inaweza kufanya kazi mara moja kwa wiki au siku za mwisho wa juma tu na sehemu nyingine inaweza ikafunguliwa mida ya jioni tu na watu wanapokezana kazi ya kuisimamia; sema kwa mfano inafunguliwa saa kumi hadi saa moja jioni.

### 6. **Kuishirikisha Jumuiya Katika Uendeshaji wa Maktaba**

Maktaba haitakuwa ya jumuiya kama haitohusishwa wana jumuiya katika uanzishaji wake, uendeshaji wake, na utunzaji wake. Hivyo ili ifanikiwe ni lazima jumuiya ihusishwe kikamilifu. Kamati inaweza kufikiria namna mbalimbali za kuishirikisha jamii zaidi ya kuitaka

kuchangia vitu au fedha. Kuandaa michezo, mashindano, masimulizi ya hadithi, michezo ya watoto n.k inaweza kuwa sehemu ya maktaba hiyo.

Mojawapo ya njia nzuri za kuishirikisha jumuiya katika uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba ni kuwa na Harambee (fundraising). Ili watu waweze kujitokeza kuchangia maktaba ni lazima waone kuwa ina umuhimu wake na kuwa fedha zao zitatumika vizuri. Tayari jamii ina michango mingi sana na ya kila namna; hivyo ili watu wachangie ni muhimu ionekane kuwa maktaba ni sehemu ambayo hawatojuta kutumia fedha zao kwani itawanufaisha wao na watoto wao.

Baadhi ya njia nzuri za kuchangishia fedha kwa ajili ya maktaba ni kama hizi:

- Tiketi za Zawadi (raffles)
- Minada – watu wanaweza kutoa vitu ambavyo vinaweza kuuzwa kwa mnada.
- Kuuza vifaa vya shule. Kama baadhi ya vifaa vinanunuliwa kwenye maduka ya jumla basi vinaweza kuuzwa kwenye jamii. Itaokoa muda wa watu kwenda mjini au maduka ya mbali kufuatilia vifaa hivyo kama wataweza kupata kwenye jamii.
- Sadaka; mojawapo ya njia nzuri hasa pale ambapo taasisi za dini zimehusishwa kunaweza kufanyika mchango wa kusaidia uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba. Watu wakijua umuhimu wake hawatoona vibaya kuchangia.
- Misaada (grants) – Hii ni misaada kutoka kwenye jumuiya yenyewe. Kuna watu wana maduka, makampuni n.k na wanaweza kutoa misaada mbalimbali ya kuwezesha kuanza kwa maktaba. Vitu kama rangi ya kupaka kontena, viti, makabati ya vitabu vinaweza kabisa kutolewa kama misaada.
- Maktaba Pacha – kuna taasisi zinazoweza kuunganisha maktaba ndogo ya jumuiya na maktaba za nchi zilizoendelea (library twinning). Ukifanikiwa kupata maktaba inayokubali kuwa pacha wa maktaba yenu, wanaweza kuwatumia vitabu na vitu vingine kwa ajili ya maktaba.

Ukitumia njia hizi na ubunifu mwingine maktaba haiwezi kukosa fedha ama za kuanzia au kuendeshea. Jambo la msingi ni kuwa tayari kuanza na kitu mkononi kama mbegu.

**MFUMO WA KUPANGA VITABU**

Mojawapo ya mambo ambayo yatahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka mara baada ya kuamua kuanzisha maktaba ya jumuiya ni mfumo wa kupanga vitabu kwenye maktaba ili watu waweze kuvifikia kwa urahisi. Iko mifumo mbalimbali ambayo inatumika rasmi au mnaweza kubuni mfumo wenu. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa mtu anapotaka kitabu akielekezwa kilipo basi akipate kwa urahisi. Hata bila ya msaada mtu aweze kupata kitabu anachotaka kwa urahisi. Jambo hili limeelezwa kwa kirefu katika kijitabu kile cha Kiingereza ambacho anayetaka naweza kumtumia kwa barua pepe.

**Mwisho**

Hizi ni hatua za msingi tu. Kwa yeyote anayetaka kujisomea zaidi katika lugha ya Kiingereza kipo kijitabu kingine ambacho kinaweza kuwa msaada kwa anayetaka kuingia kwa undani na ambaye yuko tayari kulifanyia kazi wazo hili. Kijitabu hiki kimetumiwa sehemu mbalimbali duniani kusaidia watu wanaoataka kuanzisha maktaba za jumuiya na kina mifano mingi na mawazo mengi kweli kweli. Naweza kumtumia bure yeyote anayetaka kuwasiliana name kukipata kwa njia ya barua pepe.

Katika kijitabu hicho cha jinsi ya kuanzisha maktaba ya jumuiya – ambacho mawazo yake mengi nimeyatumia hapa kwa kifupi – mambo mengi yanaongolewa kwa kina. Mambo kama jinsi ya kuzuia wizi wa vitabu, fomu mbalimbali unazoweza kutumia, masharti, na mifano mbalimbali ya nyaraka unazoweza kuzitumia kwenye maktaba yenu utaweza kuzipata. Ni kitabu kilichoko katika lugha ya Kiingereza na kilitolewa na UNESCO miaka kadhaa nyuma.

Ukiwa na maswali au kutaka ushauri au maoni hasa kama umedhamiria kuanza kitu wasiliana nami.

mwanakijiji@jamiiforums.com

www.tafakari.com

Facebook: “Mzee Mwanakijiji”

Whatsap: +1 248 904 3509